# Usawiri wa Mhusika Ngoromiko katika Ngano na Masimulizi ya Kijamii: Mifano kutoka Vijiji vya Kware na Kwasadala

*Shadidu A. Ndossa*[1] na *Maryam J. Ismail*[2]
[1]*Chuo Kikuu cha St. John cha Tanzania*
[2]*Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar*

**Ikisiri**

**Makala hii inachunguza usawiri wa mhusika Ngoromiko katika Ngano za Kichaga. Kwa jumla, mhusika Ngoromiko ni mhusika wa kufikirika anayepatikana katika ngano na masimulizi ya kijamii katika vijiji vya Kware na Kwasadala vilivyopo wilaya ya Hai-Kilimanjaro. Utafiti uliofanywa uliongozwa na malengo mawili ambayo ni kubainisha usawiri wa mhusika Ngoromiko kupitia ngano na masimulizi ya kijamii kutoka vijiji teule na, pili, kubainisha dhamira zinazowasilishwa na mhusika Ngoromiko. Mbinu ya mahojiano na ushuhudiaji ilitumika katika ukusanyaji wa data. Watafitiwa ishirini walihusika katika utafiti huu. Nadharia ya Uhalisiajabu ilitumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data. Kwa jumla, matokeo ya utafiti yanaonesha mhusika Ngoromiko amesawiriwa katika namna ya kutisha na kuogopesha na kuwa ana jicho moja, mguu mmoja na kuwa na makazi katika maeneo yenye kutisha. Vilevile, mhusika huyu amehusishwa na dhamira mbalimbali kama vile chuki, vitisho, vimbwanga vya usiku, ufantasia na kupinga usasa na kuumbatia ukale.**

**Maneno Muhimu:** *Usawiri, Wahusika, Ngoromiko, Masimulizi ya Kijamii, Ngano*

## Utangulizi na Mapitio ya Maandishi

Ngano na hadithi ambayo mara nyingi wahusika wake ni mchanganyiko wa watu na wanyama. Jamii ya Kiafrika kama zilivyo jamii nyingine duniani zimekuwa zikitumia ngano kwa minajili ya kurithisha adili za jamii na kutoa burudani kwa pamoja. Katika utunzi wa kazi hizi za kifasihi, wahusika ni sehemu muhimu sana katika kusadia kufikisha ujumbe wa mwandishi. Wataalamu mbalimbali (Mlacha, 1985, 1986, 1987, Madumulla 1987, 2009, Njogu na Chimerah, 2008, Senkoro, 2011) wameshughulikia wahusika katika fasihi ya Kiswahili na wote kwa namna moja au nyingine, wanakubaliana kuwa wahusika ni viumbe waliokusudiwa kuwakilisha tabia za watu halisi katika kazi ya fasihi. Wao ndio ambao hubeba fikra, msimamo, mtazamo na falsafa za mwandishi au msimulizi na kuziwasilisha kwa hadhira (Senkoro, 2011). Moja ya sifa muhimu inayoitambulisha fasihi ya Kiafrika na hasa fasihi simulizi ni matumizi ya wahusika wa kiajabu-ajabu. Senkoro (ameshatajwa) anaona kuwa wahusika hawa sio tu wanaogopesha bali wanawakilisha ulimwengu usioonekana ambao Waafrika wengi huamini kuwa upo. Wahusika hawa ni pamoja na mashetani, majini, mazimwi, upepo, kimbunga, mwanga, radi na hata giza. Aidha, wapo wahusika wengine kama mawe, miti, milima na majabali. Kwa pamoja wahusika hawa wa kiajabu hupewa sifa za kibinadamu na kuamiliana na wahusika wenzao kwa namna ya kustaajabisha na kushangaza.

Kwa namna hiyohiyo, mhusika Ngoromiko ni mhusika wa kutisha anayejitokeza katika ngano na masimuli ya kijamii katika maeneo mengi ya mkoa wa Kilimanjaro. Aidha, kwa namna ya kipekee mhusika huyu amekuwa akijitokeza sana katika masimulizi ya kijamii na hadithi za watoto katika vijiji tajwa. Mhusika huyu amechorwa katika namna ya kutisha na kuogopesha. Pia, amepewa uwezo mkubwa wa kufanya na kutenda ambao sio wa kawaida. Wengi wanamuona kuwa anazo sifa za kinusu-mungu na ambazo kwa kiasi kikubwa amezitumia kuwajengea woga viumbe wote wanaokutana naye.

**Kuhusu Nadharia Uhalisiajabu**

Nadharia hii pia hujulikana kama nadharia ya Uhalisimazingaombwe ni mojawapo ya nadharia za Usasa Leo ambayo huamini kwamba kazi ya fasihi huundwa kwa mchanganyiko wa matukio ya kawaida na yale yasiyo ya kawaida ambayo yote husawiri mambo yaliyopo katika jamii ya mwandishi. Kwa mujibu Strecher (1999) na Zamora na Faris (1995) nadharia ya Uhalisiajabu iliasisiwa huko Ujerumani mwaka 1925 na Franz Roh aliyekuwa mhakiki maarufu wa Sanaa katika kipindi cha zama zake. Franz ndiye alitumia istilahi ya Uhalisiajabu katika muktadha wa sanaa kuelekeza na kuonyesha jinsi ya kusawiri aina fulani ya uajabu au mazingaombwe yaliyomo kwenye uhalisi uliozoeleka. Ingawaje misingi na matumizi ya nadharia iliyobuniwa na Roh (ameshatajwa) kwa wakati huo imebadilika sana kwa wakati huu bado anaendelea kuwa mtu muhimu katika uanzishwaji wa nadharia hii. Kwa jumla, nadharia hii imekuwa ikitumika kusawiri aina ya uajabu-ajabu au umazingaombwe katika kazi mbali za fasihi na sanaa kwa jumla. Mbatiah (2002) anaeleza kuwa, istilahi hii inatumiwa kuelezea mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo na matukio ya kifantasia husawiriwa kwa kuiga mtindo wa uhalisia, yaani kwa kuyaeleza kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni mambo ya kawaida. Cooper (1998) na Strecher (1999) wanaongeza kuwa, katika nadharia ya uhaliajabu hali za kushangaza na kuogofya, huwasilishwa kana kwamba ni hali za kawaida. Wasomaji, wasikilizaji na watazamaji huelezwa mambo ya kiajabuajabu na kuaminishwa kuwa hayo mambo ni ya kawaida na yanaweza kutokea katika ulimwengu wanamoishi.

Wamitila (2008) anamuunga mkono Mbatiah kwa kudai kuwa dhana ya uhalisiajabu huhusishwa na Marekani ya Kusini au hata nchi zinazoitwa ulimwengu wa tatu. Sifa yake kuu ni kuyaeleza matukio ya kifantasia au ya kiajabuajabu na ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja, kwa maana inayoyafanya yaonekane ya kawaida. Sababu hasa ya matumizi ya mtindo huu ni kuonyesha kuwa matukio aina hii hupatikana katika maisha ya kawaida katika jamii zinazohusika. Wamitila (2008) anadai kuwa nadharia ya Uhalisiajabu hushughulikia matukio ambayo ni vigumu kuyaelezea katika msingi wa uhalisi wa kawaida katika jamii. Alexander (1990) na Chanady (1985) katika Rio (1999) wanaona kuwa, Uhalisiajabu ni kielelezo cha jinsi nadharia ya Usasa Leo inavyotulazimu kufikiria upya juu ya riwaya za kimapokeo kuhusu riwaya za uhalisia za karne ya kumi na nane na tisa. Wanaongeza kuwa Uhalisiajabu unahusu matukio yasiyo ya kawaida, ya kimiujiza au chochote kilicho kinyume cha uhalisia wa kawaida. Muhimu zaidi ni kwamba matukio yanayotendeka katika uhalisiajabu hayawezi kujitenga na uhalisia. Zipo kazi za Kiswahili ambazo zinaakisi dhana hii ya ahaliajabu. Miongoni mwa waandishi maarufu walioandika kazi zao na kuakisi nadharia hii ni S.A Mohamed; kazi zake maarufu ni pamoja na *Pungwa* (1988), *Kivuli Kinaishi* (1990) na *Amezidi* (1995).

Kwa jumla, nadharia hii imetumika katika Makala haya kuelezea usawiri wa mhusika Ngoromiko katika ngano na masimulizi ya kijamii katika vijiji vya Kware na Kwasadala. Nadharia imetumika ili kueleza kwa urahisi na kwa ufanisi nafasi ya mhusika huyu wa kimaajabu na dhana anazowakilisha kupitia uhusika wake. Hii ni kwa kuwa mhusika huyu amechorwa kwa namna ya kustaajabisha na kuogopesha. Udhati wa mhusika huyu ni wa kufikirika kwa kuwa ameendelea kuishi katika dunia ya kidhahania kuliko dunia ya kweli.

**Kuhusu Vijiji vya Kware na Kwasadala na Sampuli ya Watafiwa**

Vijiji hivi vyote vipo katika kata ya Masama Kusini, tarafa ya Masama, Wilaya ya Hai Mkoa wa Kilimanjaro. Wakazi wa vijiji hivi wengi wao ni Wachaga na wanajihusisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi kama vile kilimo cha mahindi, alizeti, maharage, mbogamboga na kahawa. Pia, wapo wanakijiji wengi wanafanya biashara kubwa na ndogondogo. Aidha, wanakijiji wa maeneo haya wanajihusisha na ufugaji mdogomdogo wa ng'ombe (wa kawaida na wa maziwa), mbuzi, kondoo na kuku. Kuhusu sampuli ya watafitiwa; utafiti uliwahuisha watafitiwa 20 kutoka katika vijiji tajwa. **Njia ya usampulishaji tajwa** (*snowballing sampling*) ilitumika katika kuwapata watafitiwa. Katika njia hii watafitiwa walipatikana kwa kutajana; yaani mtafitiwa mmoja aliyehojiwa alimpendekeza mtafitiwa mwingine ambaye aliamini kuwa anazo taarifa zaidi kuhusu kilichokuwa kinatafitiwa. Sababu kuu ya kutumia njia hii ni kutokana na mada husika ambayo inahitaji taarifa muhimu na zisizo za kawaida

ambazo sio kila mtu anazifahamu. Ni muhimu kutaja kuwa wahojiwa walipaswa kuwa wakazi wa vijiji tajwa au waliozaliwa na kuishi katika maeneo hayo kwa muda mrefu.

**Usawiri wa Sifa za Mhusika Ngoromiko**

**a) Umbile**

Mhusika Ngoromiko amefafanuliwa vema kwa kutumia umbo lake. Maelezo mengi yanayotaja muonekano wake yamekuwa yakutisha na kufunikwa na sifa za ajabu zisizo za kawaida kama inavyofafanuliwa hapo mbele.

**i) Mhusika Mwenye Jicho Moja Linalowaka Mithili ya Taa Kubwa**

Kwa kiasi kikubwa, maumbile ya mhusika Ngoromiko kupitia hadithi na masimulizi yamechorwa akiwa na jicho moja linalowaka kwa kutoa mwanga mkali mithili ya taa kubwa ya karabai. Kwa kuzingatia maeneo mengi ya vijijini hugubikwa na kiza kinene, usawiri huu unatoa ishara namna mhusika Ngoromiko anavyotisha pindi anapojitokeza kwa mwanadamu au kiumbe kingine chochote. Ni muhimu kutaja hapa kuwa, masimulizi haya ni ya kijadi na ya kimapokeo hivyo basi kufananishwa kwa uwakaji wa jicho la mhusika Ngoromiko na karabai ni jambo la kimapokeo vilevile. Hii ni kusema kuwa kwa wakati huo wa zamani taa ya karabai ndiyo taa ambayo ilikuwa na mwanga mkubwa; hivyo ukubwa wa mwanga wa karabai umefananishwa na uwakaji wa jicho la Ngoromiko. Aidha, katika baadhi ya maeneo hufaninisha mwanga unaotolewa na Ngoromiko na mwanga wa jua. Vyovyote iwavyo, masimulizi yanaonesha kuwa, moja ya utambulishi muhimu wa mhusika Ngoromiko ni jicho linalotoa mwanga mkubwa sana. Mwanga huu hubadili hali ya usiku kiasi kuwa huonekana kama mchana. Hali hii sio tu kuwa ni ya kustaajabisha na kuopesha bali humfanya Ngoromiko kuonekana kuwa mhusika ambaye sio wa kawaida katika ngano na masimulizi ya kijamii. Kwa mujibu wa Madumulla (2009), Semzaba (2006), Mlaga (2017) wahusika wa namna hii ni maarufu sana katika ngano za Kiafrika na huwakilisha dhana mbalimbali muhimu zinazoelezea falsafa ya Kiafrika kama vile nguvu za giza, vitisho, nguvu, imani na dini.

**ii) Mhusika Mwenye Mguu Moja**

Katika namna ya kustaajabisha, mhusika Ngoromiko amechorwa mara zote akiwa na mguu mmoja. Hali hii humfanya sio tu kuwa mhusika wa kustaajabiwa bali kuwatisha wale wote anaokutana nao. Katika baadhi ya masimulizi mguu wake umesawiriwa kuwa ni mrefu na anaweza kukanyaga pale anapotazama. Hii ni kusema kuwa anao uwezo wa kwenda kwa haraka masafa marefu kwa muda mfupi sana (maelezo zaidi kuhusu uwezo wa kutembea yatatolewa huko mbeleni). Ni wazi kuwa, uchoraji wa mhusika huyu kwa kumuonesha kuwa na mguu mmoja unamfanya kuonekana kuwa si kiumbe wa kawaida kwa kuwa imezoeleka kuwa, viumbe wengi huwa na miguu miwili au miguu minne. Aidha, kwa wasikilizaji wa hadithi hasa watoto hali hii pia huwastaajabisha na kuwaogopesha kwani ni wazi kuwa katika dunia wanamoishi wamezoea kuwaona viumbe wakitumia ima miguu miwili au zaidi (Madumulla, 2011 na Bakize, 2014).

**iii) Urefu Usio na Kikomo**

Aidha, wasimuliaji wengi wa hadithi za kimapokea katika vijiji tajwa wamemsawiri mhusika Ngoromiko kwa urefu usio na kikomo. Katika masimulizi mengi ya kamapokeo mhusika huyu amesilimuliwa kwa maeneo yafuatayo "…*mara kwa mbali ilionekana taa kubwa mfano wa karabai. Punde si punde hamadi, alijitokeza Ngoromiko. Alikuwa ni mrefu sana hadi kufika mawinguni…..".* Maelezo haya yanaonesha wazi kuwa mhusika huyu ana urefu usio wa kawaida. Aidha, hali hii inazidi kuonesha namna mhusika huyu alivyosawiriwa kimaajabu hali inayomfanya kuwa mhusika wa kutisha. Zaidi ni kuwa, mhusika huyu anao uwezo usiomithilika. Hii ni kwa kuwa, kwa kuwa na urefu usio na kikomo amenasibishwa na kuwa na nguvu za ajabu za kuweza kufanya kila kitu. Aidha, kupitia urefu wake anao uwezo wa kuona kila kitu akiwa katika sehemu yoyote. Kwa kawaida, hadithi za watoto zenye wahusika wenye sifa hizi za kiajabuajabu mara nyingi huwafurahisha sana na kuwavutia kuzisikiliza (Bakize, 2014 na Abdallah, 2018).

**b) Makazi ya Kutisha**

Kwa kuzingatia kuwa mhusika huyu amechorwa katika namna ya kutisha hata makazi yake mengi yameakisi hali hii. Hadithi nyingi zilizomjumuisha mhusika huyu zimemchora katika maeneo makuu matano; mosi, amechorwa kandokando ya mito au maji mengi. Pengine hali hii ni mwendelezo wa hadithi za kimapokeo ya Kiafrika na vile vya kidini ambazo wahusika wa kutisha huchorwa sambamba ya hali ya umajimaji. Inafahamika kuwa katika masimulizi mengi ya kimapokea wahusika wa kutisha, hasa majini, huhusishwa na maji; mito, mabwawa na bahari kuu (Senkoro, 2011, Bakize 2014 na Mlaga 2017). Pili, mhusika Ngoromiko amesawiriwa kuwa anapatikana na kuishi katika miti mikubwa hasa iliyopembezoni mwa mito au misitu. Kwa kuzingatia kuwa vijijji vyote viwili vinasifa zinazofanana mhusika huyu amechorwa kuwa anapenda kuishi katika miti ya **mikuyu[1].** Miti hii ni mikubwa sana na imekuwa ikihusishwa na mambo ya kutisha, hivyo basi, mhusika Ngoromiko ameendelea kuonekama kuwa mhusika anayetisha na asiye wa kawaida. Tatu, pia, mhusika Ngoromiko amehusishwa na kuishi katika maeneo ya makaburi. Ni wazi kuwa makaburini na mahali panapoogofywa, hivyo mhusika anayeswiriwa kupatikana katika maeneo haya nayye pia huonekana kama vile sio mhusika wa kawaida. Nne, mhusika Ngoromiko amechorwa kama mhusika anayepatikana katika milima. Katika vijiji tajwa mhusika amenasibishwa kutokea kwake na milima kama vile mlima Moram, mlima Luka na mlima Udoro ambayo ni milima maarufu inayopatikana katika vijiji tajwa. Ni wazi kuwa maeneo ya milima ni maeneo maarufu katika vijiji tajwa; hivyo uchoraji wa wahusika katika maeneo haya hueleweka zaidi hasa kwa watoto. Aidha, baadhi ya maeneo haya yana miti na mawe makubwa hivyo yanatisha hasa wakati wa usiku. Mwisho, mhusika huyu umehusishwa na kuishi katika mapango. Mapango haya yanapatikana katika maeneo ya vijiji na yanafahamika kwa giza kubwa lenye kutisha hasa wakati wa usiku.

**c) Sauti ya Kutisha**

Mhusika Ngoromiko amesawiria kupita sauti yake ya kutisha. Katika hali hii wasimulizi wengi wamekuwa wakimchora kuwa anao uwezo wa kutoa sauti kali mithili ya radi. Sauti hii mara nyingi huambatishwa na mingurumo/mikwaruzo mikali inayotetemesha kama alivyosimulia Fadhili[2] kwa kusema yafuatayo:

> *Ngoromiko wanaelezwa kuwa wana sauti kali sana. Wanapoitoa sauti hiyo huambatana na mngurumo mithili ya radi. Yeyote anayeisikia sauti hii huogopa na kupagawa. Kwa kuwa sauti hii huweza kusikaka mbali kabisa, Ngoromiko hutumia njia hii kuwaeleza watu kuwa nipo hapa na kuwatisha viumbe wengine hasa wanaadamu.*

Maelezo haya yanabainisha wazi kuwa mhusika Ngoromiko anayo sauti kali na inayoogofya. Aidha, ni wazi kuwa sauti yake huweza kusafiri masafa marefu na hivyo kusikiwa na watu walio mbali kabisa. Muhimu pia hapa tunaona kuwa, ukali wa sauti ya Ngoromiko inahusishwa na sauti ya kiasili yaani sauti ya radi. Pengine kwa wakati huo mlio wa radi ndiyo uliokuwa mlio mkubwa kuliko kitu kingine chochote. Chakushangaza ni kuwa pamoja na kuwa kwa sasa zipo sauti na milio mikubwa zaidi kama vile milio ya risasi, honi za treni na hata mabomu, bado masimulizi yanahusiana na mhusika Ngoromiko yameendelea kufanya tashbiha ya sauti ya mhusika huyu na mlio wa radi.

**d) Mbio za Ajabu Kama Upepo**

Sifa nyingine muhimu inayomsawiri mhusika Ngoromiko ni ule uwezo wa kusafiri masafa marefu kwa muda mfupi sana. Hadithi nyingi za kimapokeo zimemchora mhusika huyu kama mwenye uwezo

[1] Mikuyu ni miti maarufu inayomea katika maeneo yenye majimaji hasa mtoni na katika mapito ya maji. Miti hii huishi kwa muda mrefu na huwa mikubwa sana. Katika vijiji teule (Kware na Kwasadala) miti hii huhusishwa na mambo mbalimbali ya kutisha kama vile makazi ya majini na mashetani.

[2] Shabani (Shaba) Fadhili ni mkazi wa kitongoji cha Bomakati, kijiji cha Kware. Anajihusisha na kilimo na ufugaji. Maelezo haya alimpatia mtafiti nyumbani kwake mnamo tarehe 25 Agosti 2019.

wa kwenda mwendo sawa na upepo wa upepo. Wapo pia wanamhusisha na uwezo wa kupaa na kwenda mwedo wa haraka sana kama anavyosimulia Munisi[3] kwa maneno yafuatayo:

> *…walipomuona Ngoromiko katika mkuyu mkubwa waliamua kutimua mbio kuelekea nyumbani. Walitupa majembe yao na mapanga waliyokuwa wakitumia katika shughuli yao ya unyweshaji (umwagiliaji) mazao. Baada ya dakika chache walistaajabu kumuona tena Ngoromiko akiwa mbele yao…*

Maelezo haya yanatanabahisha kuwa Ngoromiko anao uwezo wa kusafiri kwa masafa marefu ndani ya muda mfupi. Aidha, maelezo haya yanashabihina sana na usawiri wa wahusika majini na mizimu katika simulizi za kimapokeo kutoka katika jamii mbalimbali za Kiafrika ambao mara nyingi husawiriwa katika namna ambayo wanaweza kusafiri umbali mrefu ndani ya muda mfupi sana (Matteru, 1983 na Senkoro 2011). Kwa jumla mhusika huyu amechorwa kwa namna ambayo anamkatisha tamaa kila atayekutana nae kuwa ni lazima asalimu amri. Ni wazi kuwa kufananisha mbio za Ngoromiko na upepo ni sawa na kusema kuwa hakuna mwenye uwezo wa kukutana naye na akaweza kumkimbia. Baadhi ya watafitiwa walieleza hali kuwa ni jumla ya vitisho vinavyowafunga watu katika ukale na kuogopa kuchukua hatua za kubadili mambo. Aidha, hali hii inaonesha namna ilivyo ngumu kubadili mambo katika jamii hasa za vijijini. Wengi wanaamini kwa yapo mambo ambayo yameumbwa kwa namna moja na hayawezi kubadilika. Mambo hayo ni sehemu ya maisha ya jamii husika ambayo hayahojiwi wala kujadiliwa na mtu yeyote. Aidha, wengine wanaona kuwa, simulizi hizi zipo maalum kwa ajili ya watoto kwa kuwa kundi hili linahiji kupewa kunga maalum za jamii yao katika umri mdogo ili watakapokuwa watu wazima waweze kuziishi, kuzilinda na kuziheshimu (Bakize, 2014 na Abdallah, 2018).

**e) Uwezo wa Kuona Mbali**

Aidha, Ngoromiko amesawiriwa kwa uwezo wake wa kuona mbali sana. Tumeshaeleza huko nyuma kuwa, Ngoromiko amesawiriwa kama kiumbe mwenye urefu wa ajabu unaokaribia mawinguni. Pia, ametajwa sana kwa uwezo wake wa kuongaza kama taa kubwa kupitia macho yake. Ukichanganya sifa hizi mbili ni wazi kuwa, Ngoromiko amechorwa katika namna ambayo anaweza kuona kila kitu kiwe karibu au mbali, kikubwa au kidogo. Aidha, masimulizi mengi ya kimapokeo yamempa sifa ya 'kutangulia kuona'- hii ni kusema kuwa watu wengi wanaomuelezea Ngoromiko huamini kuwa pale unapomuona mhusika huyu basi ujue ameshakuona muda mrefu sana. Aidha, ipo imani kuwa muda wote Ngoromiko huwaona hasa wanadamu na iwapo hajachukia basi huwa hajitokezi. Pale unapomuona basi ujue kuna jambo ambalo limemkera hivyo anajitokeza ili kuonesha hasira zake kama anavyosema Mikidadi[4] maneno yafuatayo:

> Wa*tu husema kuwa Ngoromiko anauwezo wa kukuona kabla hujamuona. Mara nyingi hujitokeza vaaap! Na kisha hukuuiliza, "je umenionea wapi?" kama utamwambia kuwa nimekuonea hapahapa basi huwa hana shida na wewe. Lakini kama utamwambia nimekuonea mbali basi hukasirika na kimo chake huongezeka maradufu…*

Maelezo haya ya Mikidadi yanataja mambo mawili muhimu; mosi, uwezo wa Ngoromiko kujitokeza kwa watu katika mazingira ya kustaajabisha. Hii ni kusema kuwa Ngoromiko hutokea 'ghafla bin vuu' na kuibua taharuki kwa watu. Pili, ni kuwa Ngoromiko huwaona watu kabla hawajamuona. Ndiyo maana hata swali analoulіza watu anataka ajibiwe kuwa hakuonwa akiwa mbali; bali ameonwa kwa karibu. Kwa tafasiri ya baadhi ya wahojiwa wetu wanaona kuwa fikra hizi zinatoa taswira katika jamii kuwa mambo mengi yanayohusiana na watu yameachiwa watu wachache tu wayatizame kwa niaba ya wengine. Jamii na hasa vijana na wanawake wamebaki kuishi katika fikra za wazee pamoja na mikatale ya kimila inayominya fikra na mitazamo mipya. Kwa jumla wengi

[3] Abdallah Munisi ni mzaliwa wa Kijiji cha Kwasadala. Kwa sasa ni mwalimu wa fasihi katika shule ya sekondari Sangara iliyopo jiji Dar es Salaam. Mahojiano haya yalifanyika Dodoma tarehe 17 Agosti 2019.

[4] Salimu Mikidadi ni mkazi wa Dodoma. Amezaliwa na kuishi kijiji cha Kware kwa sehemu kubwa ya maisha yake. Kwa sasa anajishughulisha na biashara ndohondogo katika Jiji la Dodoma. Maelezo haya aliyatoa jijini Dodoma tarehe 28.08.2019.

wanatazama kuwa mila za kizamani zinakwamisha maendeleo hasa maeneo ya vijijini ambamo watu wengi wameshikilia fikra za kizamani.

**f) Uadui na Mwanadamu**

Sifa nyingine muhimu inayomtambulisha Ngoromiko ni mapambano yake yasiyokoma na kiumbe mwanadamu. Katika masimulizi ya kijamii na hata ngano hakuna uthibitisho wowote unaomuonesha mhusika huyu akipambana na viumbe wengine zaidi ya binadamu. Daima dumu Ngoromiko amechorwa akipambana na mwanadamu. Ifahamike kuwa katika vijiji tajwa watu wa eneo hili sawa na maeneo mengine mengi ya vijiji nchini Tanzania hujihusisha na ufugaji wa mbuzi kondoo, ng'ombe, kuku, bata, mbwa, paka n.k. Pia, wapo wanyama wengine wa porini kama tumbili, swala, kima, kwale, kanga, njiwa na ndege wengine. Hivyo, ilitarajiwa kuwa mapambano ya Ngoromiko yangeweza kuwahusisha pia viumbe wengine lakini yameelekezwa kwa mwanadamu pekee. Kwa hali hii wapo wanaoona kuwa Ngoromiko ni mzimu unaopambana na mwanadamu kama kiumbe mkosaji na anayevuruga tamaduni, mila na desturi za jamii. Aidha, wapo wanaoona kuwa Ngoromiko ni kivuli cha shetani ambacho daima humtia hofu mwanadamu na kumuweka mbali na Mungu wake. Hivyo, ni wazi kuwa haitegemewi mhusika huyu ajiingize katika mapambano na wahusika wengine bali hujitahidi kumpoteza mwanadamu katika uhusiano wake na Mungu.

**g) Ujitokezaji wa Usiku**

Masimulizi yote yanayomhusu Mhusika Ngoromiko yamesawiriwa wakati wa usiku. Vivile, ujitokezaji wake umeambataishwa na giza nene tena usiku mkubwa (kuanzia saa 7 usiku mpaka 11 alfajiri). Inafahamika kuwa muda huu watu wengi huwa wamelala na giza huwa limetanda. Maandishi mengi ya kifasihi na ya kidini yanauhusisha muda huu na dunia ya giza inayotawaliwa na viumbe vya kutisha kama mashetani, majini na mizimu. Pengine ndiyo maana mhusika Ngoromiko naye amechorwa kama mhusika anayejitokeza na kutamba muda huu. Pia, watu waliohojiwa walimueleza mtafiti kuwa, Ngoromiko hujitokeza usiku kwa kuwa sio kila mtu anaweza kumuona; bali ni watu maalum ndio ambao humuona. Wapo pia wanaoamini kuwa Ngoromiko hulala wakati wa mchana na inapofika usiku ndiyo hufanya shughuli zake. Hivyo, wale ambao hukutana nae ni sawa na watu waliongia katika himaya isiyowahusu. Almuhimu, Ngoromiko amesawiriwa kama kiumbe cha usiku ambaye huitumia taa yake kuona kila kitu na kuwatisha wale wote wanakatiza katika himaya yake. Zaidi ya hapo, wapo wahojiwa ambao wanaona hali hii ya ujitokezaji wa Ngoromiko wakati wa usiku inaakisi hali ya mapambo ya kujificha na kutojitokeza hadharani. Wanalinganisha hali hii na kukumbatia mila, tamaduni na desturi zisizofaa ambazo zimeendelea kufanyika katika giza kwa kujificha. Wanalinganisha hali hii na mila kama vile ukeketaji, unyanyasi wa mwanamke na mauaji ya albino; mambo haya hayafai lakini hufanyika kwa kujificha gizani kwa sababu mbalimbali tena zisizo na msingi.

**Dhamira Zinazowasilishwa na Mhusika Ngoromiko**

Kupitia masimulizi yanayomsawiri mhusika Ngoromiko yapo mambo mengi ambayo hadhira hujifunza. Badhi ya mambo haya ni kama ifuatavyo:

**a) Umazingaombwe**

Maelezo yote yanayofafanua kuhusu mhusika Ngoromiko ni ya kimazingaombwe. Mhusika huyu na maelezo yote yanayomhusu yamekaa kimaajabu na hayawezi kushikika katika ulimwengu wa kawaida. Ni sawa kusema kuwa mhusika huyu ni kama mhusika wa kufikirika anayeishi katika dunia ya maajabu tu. Aidha, pamoja na kuwa mhusika huyu ametajwa katika masimulizi ya kihadithi na yasiyo ya kihadithi bado hakuja na ushahidi usio na shaka kuwa ni kweli amewahi kuonekana kwa jicho la kawaida. Inawezekana kabisa mhusika huyu amechotwa kutoka katika masimulizi ya kihadithi na kuwekwa katika masimulizi ya kijamii; ambayo yanahusishwa na matendo ya dhati yanayotokea siku hadi siku. Madumulla (2009) na Mlaga (2017) wanaona kuwa fasihi simulizi imeathiri na kuathiriwa na masimulizi ya kijamii kwani zimekuwa zikitoshelezana na kujazilizana. Aidha, kwa mujibu wa nadharia ya Uhalisiajabu ni wazi kuwa msanii anao uhuru wa kuwachora

wahusika wao kimaajabu na kuwapa majukumu ya kawaida kwa minajili ya kuiaminisha hadhira yake kuwa wahusika hao ni wa kweli wanaishi katika ulimwengu wa kawaida.

**b) Ulimengu wa Fantasia**

Wamitila (2003) anasema kuwa fantasia ni dhana inayotumiwa kuelezea kazi ya fasihi ambayo inakiuka uhalisia. Maelezo haya yanaungwa mkono na Ngugi, Lyimo na Bakize (2019) ambao wanaona kuwa fantasia ni hali ya kuwapo mambo ya ajabuajabu au ya kinjozi katika kazi ya fasihi. Aidha, wanaendelea kusisitiza kuwa ufantasia unaopatikana katika fasihi andisi ni malighafi ya fasihi simulizi. Mhusika Ngoromiko anasiriwa katika ulimwengu wa maajabu na unaoshangaza mno. Kwa jumla sifa muhimu ya mhusika huyu ni maisha yake ambayo yamesanwa katika namna ya kushangaza na kustaajabisha. Ukimtazama kuanzia uwezo wake wa kusafiri kama upepo, kuangaza kwa jicho moja, kutembea kwa mguu mmoja na kuishi katika maeneo ya kutisha, ni wazi kuwa mhusika huyu anastaajabisha. Muhimu cha kutaja hapa ni kuwa mhusika huyu amesawiriwa sana katika ngano za watoto ambazo moja ya sifa yake muhimu ni ufantasia; yaani ule umaajabu wa wahusika wake. Katika hali hii watoto hupenda kusikia sifa za ajabu na za kinusu-mungu; hali ya kutoshindwa na kuweza kila kitu. Kwa hakika hali hii ni kiwalishi cha nadharia ya uhalisiajabu unaosisitiza kuhusu hali ya kuwapo kwa wahusika wanaofanya mambo ya kufikirika na ambayo hayawezi kutokea katika ulimwengu unaoshikika. Mara nyingi wahusika hawa hutumika sana katika kazi za watoto kwa lengo la huwafurahisha watoto. Wapo wanaoamini kuwa watoto huamini kabisa kuwa wahusika hawa ni wa kweli na kuwa wanaishi katika ulimwengu unaoshikika.

**c) Huwakilisha Chuki, Vitisho na Mabavu**

Mhusika Ngoromiko kwa kiasi kikubwa amechorwa kuwakilisha chuki na mabavu. Kama ilivyoelezwa huko nyuma mhusika huyu ameonekana kuzua tafrani kwa yeyote anayekutana nae. Ingawaje wapo wanaona kuwa mhusika huyu huwashambulia na kuwatisha wakosaji, uchunguzi unaonesha wazi kuwa bado hakuna yeyote ambaye amesalimika anapokutana na Ngoromiko. Kila aliyekutana na mhusika huyu alitaharuki, alikimbia na kuchanganyikiwa. Pia, hapakuna simulizi lolote liwe la kijamii au la kimapokea linaloonesha kuwa Ngoromiko anao usuhuba mzuri na wale anaokutana nao. Kwa hali hii ni wazi kuwa mhusika huyu amesawiriwa katika namna ya kuchukiza, kuogopesha na kutumia mabavu kwa kila anayekutana nae. Kadhalika, hii inapewa nguvu na namna watafitiwa wengi wanavyomhusisha mhusika huyu na mambo maovu kama vile kukumbatia mambo ya kale na kutokubali mabadiliko. Pia, wapo wanaoona kuwa Ngoromiko ni muwakilishi wa mila zinazowanyima fursa watoto, wanawake na vijana katika majukwaa muhimu ya kifamilia na kijamii.

**d) Uwakilishi wa Mila na Desturi Zisizobadilika**

Wapo wanamhusisha mhusika Ngoromiko na taswira ya kuukumbatia ukale na kupinga usasa. Wanaomini katika hili wanaona kuwa, Ngoromiko anawakilisha ukale. Pia, wanaona kuwa hakuna dhima ya muhimu ambayo mhusika Ngoromiko amekuwa akiiwakilisha yenye sura ya uchanya. Ndio maana mhusika huyu amechorwa na kupewa sifa za kinusu-mungu; ambapo hakuna kinachomshinda. Wanaona kila kitu, anasikia kila kitu, anakimbia kwa kasi isiyosemekana na anaweza kutoa ukulele unaoweza kumtetemesha kila mtu. Hivyo basi, wanahitimisha kuwa Ngoromiko ni taswira halisi ya wale wote wanaowaaminisha watu kuwa mambo hayawezi kubadilika katika jamii. Vilevile, wanaamini kuwa wale wote wanaopinga mambo ya kale wanaweza kushughulikiwa na nguvu ya kijadi ambayo haizuiliki kama anavyosema Jasmin[5]:

> *Ngoromiko ni hadithi tumeisikia sana tulipokuwa watoto. Ukweli wake ni wa kutia mashaka. Mimi naona wazee waliamua kututisha na kutuzuia kufanya baadhi ya mambo kwa maslahi yao. Kama ni hadithi ya kweli mbona mimi sijakutana nae na napita huko*

[5] Jasmin Ulomi (Mama Sofia) ni mkazi wa Kware. Amezaliwa Kijiji cha Mbwehera na kuishi kijiji cha Kware kwa sehemu kubwa ya maisha yake. Kwa sasa anajishughulisha na biashara ndohondogo ya samaki huko Kware. Maelezo haya aliyatoa Kware tarehe 2.08.2019.

*mtoni kila siku? Haya ni mambo ya kukumbatia tu mila….sawa tu nay ale ya kurithi mke, kukeketa watoto. Ni mila tu hizi na hazina ukweli.*

Maelezo ya Jasmin (Mama Sofia) yanafungua ukurasa mwingine kuhusu uwakilishi wa mhusika Ngoromiko. Kwa jumla maelezo haya yanadokeza mambo matatu muhimu. Mosi, maelezo haya yanaonesha wazi kuwa Ngoromiko ni mhusika wa hadithi tu yaani haishi katika ulimwengu wa kweli. Kinadharia maelzo haya yanasadifu msingi muhimu wa uhalisiajabu ya kuwa kuwapo kwa wahusika na matendo yasiyo ya kawaida. Pili, Mama Sofia anadokeza anaona kuwa mhusika Ngoromiko anawakilisha mambo maovu ya kimila. Mara zote wahusika hawa manaotumia ubavu, vitisho na hila kuwaogofya wanajamii kwa maslahi ya wachache. Mwisho, Mama Sofia anamuona mhusika ni mwakilishi wa viongozi waovu ambao wanasimamia mila, desturi na matendo yasiyofaa katika jamii kwa njia ya vitisho na ulaghai. Kwa jumla mambo yote matatau yanayojitokeza katika nukuu hii ni ya muhimu sana kwa kuwa yanasadifu kabisa dhima ya fasihi (iwe simulizi au andishi) ya kushajiisha maadili mema kwa jamii na kupinga uovu, uonevu pamoja na mila na desturi potofu.

### e) Usiku na Maajabu Yake

Mhusika Ngoromiko amesawiriwa katika namna ambayo anauonesha usiku, vituko na maajabu yake. Imeelezwa huko nyuma kuwa mhusika huyu amechorwa katika namna ambayo hujitokeza wakati wa usiku tu. Katika uchoraji huu yanabainika mambo yafuatayo: Mosi, mhusika huyu haonekani na watu wote kwa kuwa muda huo watu wengi huwa wamelala. Hii ni kusema kuwa, ijapokuwa masimulizi ya mhusika huyu yametapakaa kwa watu wengi wa vijiji teule bado kuonekana kwake ni kwa kimapokeo zaidi. Pili, mhusika huyu ni muendelezo wa hadithi za kutisha na matendo ya ajabu yanayotokea usiku. Inafahamika kuwa kazi nyingi zinazozungumzia ulimwengu wa mizimu, majini na masheteani huhusishwa na usiku pamoja na giza. Pia, yapo masimulizi ya watu kuchukuliwa msukule au kufanywa vizuu (Rejea *Ngoma ya Ng'wanamalundi na Dunia Uwanja wa Fujo*) ambapo matendo yake mengi hauambatana na giza. Almuhimu hapa ni kuwa usiku umevishwa matendo ya ajabu ambapo Ngoromiko hujitokeza na kutamba bila woga.

### Hitimisho

Ngoromiko ni mhusika wa ajabu anayepatikana katika ngano na masimulizi ya kijamii yanayopatikana katika kijiji cha Kware na Kwasadala. Dhima anazosimimia ni nyingi na jamii ina mitazamo tofauti kuhusu usawiri wake hasa katika yanahusiana na fasihi. Bado tafiti zinahitaji kuhusu mhusika huyu na dhima yake katika masimulizi tajwa. Aidha, mhusika huyu amesawiriwa katika namna ya kutisha na amejengewa uhasama wa kudumu baina yake na mwanadamu. Kwa kuwa amepewa sifa za kinusu-mungu mhusika huyu amechorwa kama mhusika tishio na 'anaempelekesha puta" mwanadamu. Watafitiwa wengi wanamuona mhusika huyu ni mwakilishi muafaka wa mila, desturi na tamaduni mbaya za kale zinazomnyima fursa mwanadamu kupiga hatua muhimu za kuuchumi kijamii, kitamaduni na kisiasa. Pamoja na usawiri hasi ya mhusika huyu bado simulizi la Ngoromika lipo katika jamii. Bila shaka kuendelea kwa simulizi hili ni kielelezo kingine kingine cha umuhimu wake hasa kwa wale wanaoamini kuwapo kwake na umuhimu wake kwa jamii.

### Marejeleo

Abdallah, S. (2018). "Nafasi ya Fasihi ya Watoto ya Kidijiti katika Kukuza Fasihi Simulizi: Mifano Kutoka katika Vibonzo Jongevu" Tasnifu ya Kukamilisha Mahitaji ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).

Bakize, L. H. (2014). *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Dar es Salaam: Maccony Printing Press.

Chanady, A. B (1985). *Magical Realism and the Fantastic*. New York: Garland

Madumulla, J. S. (2001). Hali ya Vitabu vya Watoto katika Tanzania. Katika *Swahi1i Forum,* Juzuu ya 8, Uk. 171-183.

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Ltd.

Madumulla, J. S. (1987) "Maendeleo ya Wahusika katika Riwaya ya Kiswahili Tanzania" Kiswahili, Juzuu 54/1&54/2, uk 66-76

Matteru, M. D. (1983). Fasihi Simulizi na Uandishi wa Kiswahili. Katika *Fasihi: Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III: Fasihi* Uk.26-37.

Mbatia, M. (2002). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks.

Mlacha, S.A.K. (1985) "Wahusika katika Riwaya za Kiswahili Tanzania 1970- 1982," Mulika Na 27, uk 29-45

Malacha , S.A.K (1986) "The Identification of Personality Differences in Kiswahili Prose Fiction" Kiswahili, Juzuu 53/1 & 53/2, uk 146-167

Malacha, S.A.K (1987) "Aggression as a Mental and Social Disorder: A Study of Swahili Novels" Kiswahili, Juzuu 54/1 & 54/2, uk 77-91

Malacha, S.A.K (1986) (1991) "Point of View as a Stylistic Device in Kiswahili Novels" Kiswahili, Juzuu 58, uk 54

Mlaga, W. K. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21*. Dar es Salaam: Heko Publishers Ltd.

Mohammed, S. A. (1990). Kivuli *Kinaishi*, Nairobi: Oxford University Press.

Mohamed, S.A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili*. Nairobi: EAEP.

Mohammed, S. A. (1995) *Amezidi*, East African, Nairobi: Educational Publishers.

Mohammed, S. A. (1998), *Pungwa*, Nairobi: Longman. Publishing, Inc.

Njogu, K. & R, Chimerah, (2008) (Toleo la Pili). Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Ngugi, P. M. Y., Lyimo, E. B na Bakize, L. H. *Fasihi ya Kiswahili ya Watoto: Maendeleo, Nadharia, Mbinu na Mifano ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: TUKI.

Rio, F. (2002). *Margical Realism Definitions*. Imepakuliwa katika Intanet (Haijachapishwa).

Semzaba, E. (2006). *Tamthilia ya Kiswahili* (Tol 2). Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTU.

Strecher, M. C (1999). Magical Realism and the Search for Identity in the Fiction of Murakami Haruki, *Journal of Japanese Studies*, Volume 25.

Wamitila, K. W; (2008): *Kanzi ya Fasihi-Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi. Vide

Wamitila, K.W. (2002). Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi. Nairobi: Focus Books

Limited.

Wamitila, K.W. (2002). Uhakiki *wa Fasihi Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Zamora, P. L. na Faris, B.W (1995). *Margical Realism Theory: History Community*. London: Duke University Press.